

KUANZISHA JAMII YAKO MPYA YA KIMISHENI



HATUA

1

CHAGUA



Wapi? Jamii iliyo karibu na wewe inayomhitaji Yesu.



Nani? Mtu wa amani wa kukuunganisha na jamii




Pamoja na nani? Timotheo wa kumkuza kwa ajili ya uzidishaji.

2

ONYESHA

Shiriki sinema ya JESUS na kikundi cha watu 10 au zaidi na uwaalike kurudi ili wajifunze kuhusu Yesu.



3


ANZA

Anza mkutano na jamii yako ya kimisheni ukitumia mchakato wa kufunza uanafunzi wa theluthi tatu- 3/3.

4

ZIDISHA

Mtume Timotheo wako kuanzisha Jamii yake binafsi ya Kimisheni.



MANENO MUHIMU

MTU WA AMANI

Mtu anayeheshimika, mwenye msukumo wa kiroho na aliye tayari kuwaalika marafiki na familia ili watazame sinema ya YESU. (Luka 10:6)


TIMOTHEO

Muumini anayefundishika, mwaminifu na aliye tayari kuzidisha Jamii ya Kimisheni. (Timotheo 2:2)

JAMII YA KIMISHENI

Jamii ya kiroho yenye ukubwa wa familia ya ndugu na jamaa, inayokua na kufanya kazi ili kujizidisha kwa kuanzisha jamii mpya za kiroho.

MUUNDO WA UANAFUNZI WA 3/3 KWA AJILI YA MKUTANO WA KIMESHENI WA JAMII



Kutazama Nyuma

Kutazama NYUMA kunamaanisha kujenga jamii kupitia kujaliana huku mkisherehekea uaminifu wa Mungu na ukuaji wa kila mmoja.

Kujaliana

Shirikini masuala ya maisha yenu (Masuala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho n.k.) na muombeane.



Ibada

Msifuni Mungu kwa nyimbo, ala, kucheza au shuhuda.



Kuwasilisha Maono

Shirikini jinsi mnavyoweza kuwa wafuasi bora wa Yesu na kile ambacho jamii yenu inaweza kufanya ili kuwafikia wengine kwa ajili ya Kristo.



Kudumisha Uwajibikaji

Shirikini jinsi mnavyoendelea katika kutii Neno na kufanya wanafunzi.



Kutazama Juu

Kutazama JUU kunamaanisha kusikia kutoka kwa Mungu pamoja. Ukitumia tableti au simu yako mahiri, tazama klipu inayofuata kutoka katika filamu ya YESU na uijadili.

HATUA

1

Onyesha: Tazama sehemu hii mara mbili.



2

Tangaza: Mwombe mshiriki wa kikundi asimulie habari hiyo kwa maneno yake mwenyewe.



3

Kamilisha: Ruhusu kikundi kijaze mapengo yoyote katika habari hiyo au wafanye masahihisho yoyote.



4

Jadili:

- Je, ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hii?
- Je, tunaweza kujifunza nini kuhusu Mungu katika habari hii?
- Je, tunaweza kujifunza nini kuhusu wanadamu katika sehemu hii?
- Je, kuna kanuni au amri ya kutii?
- Je, kuna dhambi ya kuepuka?
- Je, kipo kielelezo cha kufuata?



Kutazama Mbele

Kutazama MBELE kunamaanisha kujiandaa kwa ajili ya misheni kwa kutumia somo husika, kufanyia mazoezi habari husika na kuomba pamoja.

Kutendea Kazi

- Shirikini katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mwikie kile mlichojifunza leo.
- Fikiria kuhusu mtu katika jamii yako ambaye anahitaji kusikia habari ya leo.



Kufanyia Mazoezi

- Ambianeni habari ya leo.



Waalike

- Shiriki habari ya leo na wengine na uwaalike kuhudhuria mkutano wenu wa kikundi unaofuata.



Omba

- Mshukuru Mungu kwa kile mlichojifunza.
- Ombea wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

